



Kwa:
Jumuiya za Diaspora Duniani

**YAH: KONGAMANO LA PILI LA KIMATAIFA LA FURSA ZA UWEKEZAJI ZA TANZANIA NA UZINDUZI RASMI
WA BARAZA LA DIASPORA LA WATANZANIA DUNIANI-TDC GLOBAL**

Baraza la Diaspora la Watanzania Duniani (TDC Global) kwa kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania katika nchi za Skandinavia Baltic na Ukraine. Linayo furaha kubwa kukufahamisha kwamba kutakuwa na Kongamano la Kimataifa la kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo Tanzania litakaloendana na Uzinduzi rasmi wa Baraza la Diaspora la Watanzania Duniani (TDC Global) Tarehe 09 na 10 April 2019 Mjini Stockholm Sweden.

Kongamano litafanyika katika ukumbi uliopo kwenye meli ya Tallink Silja AB, itakayosimama katika bandari Värtahamnen yenye anwani ifuatayo :

Hamnpirsvägen 10,
S-102 53. Stockholm,
Sweden.

Simu: +46 (8) 666 33 88 (Piga namba hii kwa maelekezo zaidi)

Tarehe 09 April 2019, Itakuwa ni siku ya Kongamano la Fursa za uwekezaji nchini Tanzania. Mkutano huu utaanza saa nne na nusu asubuhi (10:30 am) na kumalizika saa kumi na dakika arubahini na tano jioni (16:45pm). Baada ya mkutano kumalizika Meli itaanza kuondoka bandarini ya Värtahamnen Stockholm Sweden na kueleka Tallin Estonia. Kutakuwa na shughuli mbali mbali za burudani na mikutano mingine ya kibiashara wakati meli ikiwa safarini usiku huo wa tarehe 09 April 2019.

Tarehe 10 April 2019 Itakuwa ni siku rasmi ya mkutano wa uzinduzi wa TDC Global. Mkutano huo utaanza saa nne na nusu asubuhi (10:30am) na kumalizika saa kumi jioni (16:00 pm) kuna uwezekano wa kuwa na mabadiliko ya ratiba. Katika mkutano huo kutakuwa na majadiliano ya kina na kupokelewa kwa hoja za Diaspora kuhusu vikwazo na njia mbalimbali za kutatua vikwazo hivyo vinavyowakabili Diaspora wa kitanzania Duniani kote.

Mkutano unategemewa kuhudhuriwa na Viongozi mbalimbali wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Viongozi Wakuu wa Baraza la Diaspora la Watanzania Duniani (TDC Global), Viongozi wa kamati zote za Baraza la Diaspora la Watanzania Duniani (TDC Global), Viongozi wa vyama mbalimbali vya Diaspora wa Tanzania na wanadiaspora toka pembe zote za dunia.



Kwa wale mnaotoka nje ya Sweden na mnategemea kufika Stockholm tarehe 09 April 2019 tunawashauri;

1. Endapo utashukia uwanja wa ndege wa Alranda Stockholm tunakushauri uchukue ndege itakayofika kabla ya saa mbili asubuhi. (08:00am). Usafiri wa rahisi na wa haraka kutoka kiwanja cha ndege kwenda mjini Stockholm ni kutumia basi la kampuni ya flygbusarna (**Airport Coaches**). Ukifika kituo kikuu cha mabasi Stockholm panda treni ya chini ya aridhi inayoelekea Ropsten (**line number T13**) na Kushuka kituo kinaitwa **Gärdet**. Kutoka hapo hadi kwenye meli takribani mita 300.
2. Endapo utashukia uwanja wa ndege wa **Skavta** Stockholm, tunakushauri uchukue ndege itakayofika kabla ya saa moja asubuhi. (07:00am). Usafiri wa rahisi na wa haraka kutoka kiwanja cha ndege kwenda mjini Stockholm ni kutumia basi la kampuni ya flygbusarna(**Airport Coaches**). Ukifika kituo kikuu cha mabasi Stockholm panda treni ya chini ya aridhi inayoelekea **Ropsten (line number T13)** na Kushuka kituo kinaitwa Gärdet. Kutoka hapo hadi kwenye meli takribani mita 300.

Kwa wale watakaopenda kutalii kidogo mjini Stockholm na kufurahi baada ya kongamano basi tunawashauri wafanye maandalizi ya hotel kwa tarehe 11 April 2019 na kuendelea kulingana na mahitaji yao. Pia mnaweza kutembelea www.hotel.com na kuchagua hotel za mjini Stockholm.

Kufanya usajili kwa ajili ya kongamano na kulipia chumba na huduma nyingine wakati wa kongamano tafadhari bonyeza link hii <https://tdcglobal.org/tdc-launch-conference/> maelezo yote muhimu utayakuta wakati unafanya usajili wako. Watu wanaweza kuwa group la watu wanne (4)na kulipia chumba kimoja chenye vitanda 4 na kuokoa pesa kwa kulipia kila mtu chumba chake. TDC Global imeandaa kongamano hili bure na hakuna malipo yeyote utakayolipa yanayokwenda kwa TDC Global.

Maelezo zaidi na matangazo mbalimbali yatakuwa yanaendele kutolewa kadri inavyohitajika kuhusiana na kongamano hili. Hata hivyo unaweza kupiga simu namba +4747262181 na +46739484288. Au Tuma barua pepe kwa info@tdcglobal.org kwa msaada kuhusiana na kongamano hili.

TDC Global inawaomba Viongozi wote kusambaza ujumbe huu kwa Diaspora wote popote walipo, ili taarifa hizi ziwafikie kwa wakati na waweze kujipanga vyema kuhudhuria kongamano hili. Mnarusiwa kusambaza barua hii katika mitandao yenu kwa kadri mtakavyoona inafaa.

Kwa wale wanaohitaji Viza,TDC Global itatoa mialiko ya Viza kwa kila mwanadiaspora atakayekamilisha kujisajili kuhudhuria na kukamilisha malipo ya malazi na chakula kwa siku hizo mbili. (2)

Asanteni.

”PAMOJA TUNAWEZA – MTU KWAO NDIO NGAO”

BARAZA LA DIASPORA LA WATANZANIA DUNIANI

NyagabonaGK

Adolph Makaya
Katibu
TDC Global
2019-01-10

